JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu 0756275058/0718406870

Mkuu wa shule: DELIGO LUPOLA

Makamu Mkuu wa Shule: KOSTANTINO SIMCHIMBA

Patron: JUSTIN MWANAWIMA.

SHULE YA SEKONDARI KIPETA,

S.L.P 78,

SUMBAWANGA.

28.3.2022.

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi:

……

S.L.P ……..……

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIPETA HALMASHAURI YA WILAYA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA MWAKA 2022

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022 kwa tahasusi ya HGL. Shule ya Sekondari Kipeta ipo umbali wa kilometa 176 Mashariki mwa mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi cha Sumbawanga. Nauli ni shilingi 25,000/= hadi kipeta sekondari kutoka Sumbawanga mjini. Kwa wanaotokea stendi kuu ya mabasi Mbeya watashukia kituo cha mabasi Mlowo iliyoko mkoa wa Songwe wilaya ya Mbozi kabla ya kufika Vwawa. Nauli ya kutoka Mlowo hadi Kilyamatundu mahali shule ilipo ni Tshs. 10,000/=. Ukifika stendi ya mabasi ya Kilyamatundu unatakiwa kupanda pikipiki (bodaboda) hadi shule Tshs. 1,000/= (kwa wanaotokea Mlowo). Njia ya Mlowo ni rahisi na gharama nafuu kuliko nyingine zote.

Muhula wa masomo unaanza tarehe …….... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe …….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …….. Wasiliana nasi kwa namba za simu zifuatazo ukipata changamoto yoyote: 0756275058/0718406870- Mkuu wa shule au 0768060850-Makamu mkuu wa shule

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

1.1 Sare za shule

a) Sare ya shule hii ni suruali mbili (damu ya mzee na dark-blue) mashati mawili meupe mikono mirefu kwa wavulana. Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta 2 rangi ya blue na tracksuit pair moja kwa wavulana.
b) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
c) Soksi jozi mbili Nyeusi za shule.
d) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
e) Sweta pair 2 (damu ya mzee 1 na darkblue 1) – ingawa siyo lazima kwa sababu kuna joto.
f) Nguo za kushindia (shamba *Dress*) suruali 1 kijani kibichi na T-shirt ya kola (form six) ya blue yenye kola nyeupe na ufito mweupe mwishoni mwa mikono au T-shirt 1 ya blue ya round kola.
g) Tai 2 (dark blue 1 na damu ya mzee 1)

1.2 Ada na michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni, unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba 62101100065 (KIPETA SECONDARY SCHOOL) katika Benki ya NMB (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip na uje na payslip orginal).
b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni :-
    i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
    ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
    iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
    iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
    v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule.
    vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya matibabu ikiwa shilingi 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na Bima ya Afya Tshs. 5,000/=.

Kama mwanafunzi ana bima atatoa shilingi 5,000/= ya huduma ya kwanza.

vii. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa) .

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Ream 1 ya karatasi (kwa mwaka)

(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (HGL)

(iii) Non programmable calculator 1.

(iv) Godoro 1 foot mbili na nusu.

(v) Mashuka pair 2 (rangi ya pink), foronya 1 (rangi ya pink) na chandarua 1.

(vi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na Kikombe)

(vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.

(viii) Kwanja 1, jembe1, reki1, mfagio 1 wa ndani na mfagio 1 wa nje.

2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya Sekondari Kipeta inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

i. **Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima**
ii. **Mahudhurio mazuri katika kila shughuli utakazopewa ndani na nje ya shule**
iii. **Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation)**
iv. **Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa**
v. **Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.**
vi. **Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.**
vii. **Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.**
viii. **Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.**

3. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(ix) Uvutaji wa sigara.

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

NB: 1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa na Results slip original ili kujua uhalali wake kwa kutumia taarifa hizo.

2. Shule itafunguliwa baada ya kupata maelekezo toka serikalini.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule :

Jina la Mkuu wa Shule :DELIGO LUPOLA.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIPETA
S.L.P.78 SUMBAWANGA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

KIPETA HIGH SCHOOL
P.O. BOX 78,
SUMBAWANGA.
DATE……

MEDICAL OFFICER
……
……
……

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR……
(NAME OF STUDENT)

Please examine the above named as to his/ her fitness as indicated below. Arrange the necessary treatment so that the certificate may be brought to school by the student.
This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a recognized Government hospital.

1. Hemoglobin ……
2. P.V Blooding ……..
3. (a) Blooding ……...
(b) Hearing ……
4. Blood pressure ……...
5. Stool for routine examination ……...
6. Urine for sugar ……...
7. Skin diseases ……..
8. Leprosy ……
9. Pulmonary tuberculosis ……
10. Asthma ……
11. Epilepsy ……..
12. Deformity ……
13. Mental problem ……
14. Comment…… ……

Name of medical officer…… Signature…… Date……
Official stamp